

Pambazuko


Toleo Namba 065

Jumatatu Machi 11-17 2024

Arusha yampa ushindi Miss World UK. 19

Mpasuko Z'bar

• ACT wajipanga kususia serikali



'Msimchoshe Rais
Samia kwa usanii'

UK. 5



Jicho la Tai

UK. 6
Ruto katikati
ya kashfa,
Bunge kujadili



UK. 8
TZ yashinda
kesi. Kulipwa
mabilioni



JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Rais Samia achukue hatua wanaomharibia

RAIS wa Tanzania Samia Suluhu Hassan mpaka sasa akiwa anakaribia kufikisha miaka mitatu akiwa madarakani, anathibitisha kwamba anaweza kufanya vyema zaidi katika utendaji wake kuongoza nchi.

Ni kutokana na 'staili' ya uongozi wake, idadi kubwa ya Watanzania wanaendelea kujenga imani naye.

Hata hivyo, huenda imani ya wananchi wake ikafifia ikiwa ataendelea kukaa kimya bila kukemea wenye kutaka kumharibia, kwani watu wengi wanashuhudia namna baadhi ya wasaidizi wake wanavyoshindwa kwenda naye katika kutatua shida za wananchi.

Wenye kutaka kumharibia Rais Samia wapo wengi; miongoni mwao ni watendaji wabovu katika ofisi za kutoa huduma kwa wananchi, hasa za serikali, halmashauri na kwenye taasisi za umma ambako wananchi wanapaswa kuhudumiwa vyema.

Katika ofisi nyingi za kutoa huduma kwa wananchi, sasa zimekuwa na watendaji wengi wa hovy, wavivu, wanatumia muda na rasilimali za serikali kufanya mambo yao binafsi.

Pambazuko limepokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi ambao wanahoji – “kulikoni?” Kwamba nini kimetokea hadi watendaji waliokuwa na nidhamu ya kazi, kuwajibika, kujituma na kuhudumia vyema wateja wao- wananchi, sasa wamebadilika!

Mbali na kuwajibika ipasavyo, malalamiko hayo mengine yanadai kuwepo ongezeko la rushwa, kwamba watendaji wengi wa serikali sasa hawana woga wa kuomba rushwa ili kutoa huduma kwa wananchi.

Je, nani amewaambia kuwa Rais Samia ni mpole kiasi cha kufumbia ujinga huo wa kudai rushwa kana kwamba ni haki yao kabla ya kutoa huduma, tena nyingine zikiwa bure kabisa!

Wapo wanaoenda mbali zaidi na kueleza kwamba huenda kauli ya Rais Samia kwamba “kila mbuzi hula kwa urefu wa kamba yake,” umechukuliwa kama ruhusa ya kuikumbatia rushwa?

Sisi katika Pambazuko hatuamini kauli hiyo ya Rais Samia kama ilikuwa ni fursa ya kuruhusu watendaji wa serikali kuitumia kuomba rushwa ili kutoa huduma kwa wananchi.

Tunaamini tu kwamba wanaoichukua kauli hiyo kuwa ruksa, ni wale wenye hulka ya rushwa na kamwe siyo msukumo wa kauli hiyo unaowafanya kuomba rushwa kana kwamba ni haki yao ya msingi kabla ya kutoa huduma kwa wananchi.

Kikubwa ambacho Rais Samia anapaswa kujiepusha nacho, ni kuhakikisha kuwa wasaidizi wake anawafuatilia kwa karibu kwa kutumia vyombo vyake vingi; vya wazi na hata vile vya sirini ili kuhakikisha wale wote wenye lengo la “kumharibia” wanajulikana na kudhibitiwa mapema kabla madhara hayajawa makubwa au kuota mizizi.

Ni muda muafaka sasa kwa Rais Samia kuwadhibiti wote wenye malengo mabaya – hasa wanaomharibia, na wale wanaoshindwa kuwatumikia wananchi ipasavyo.

Kuchukua hatua ni sasa ili kukomesha uzembe na kuimarisha imani ya Watanzania kwa kiongozi wao.

UGALI NA ELIMU...



Kila Jumamosi, katika Ofisi za Shamba la Malembo, Dar es Salaam, watu hukutana kujadili namna kilimo kinavyoweza kumkomboa Mtanzania kuondokana na umasikini. Makutano hayo, maarufu kwa jina la Jukwaa la Kula Ugali na Elimu, hudhaminiwa na mkurugenzi wa shamba hilo, Lucas Malembo. Washiriki hula ugali asubuhi huku wakijadili. (Picha kutoka Ukurasa wa X wa Malembo)

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Kila mtu anaweza kufanya chochote, na muda ukifika hakuna wa kuzuia kutimia kwa ndoto zake - kwa kadri alivyopangiwa na Mungu. Hivyo, tusidharauriane - Samia Suluhu Hassan, Rais wa Tanzania.

Tangazo

Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliwaomba kuchagua, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023

Changia Pambazuko liendelee

WAJUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufurahia kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakitumia fedha, muda, ujuzi na rasimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokua zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukuza Kiwahili, kuhabarisha, kupata maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeweza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yamewekwa wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majeraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kuimarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kuuza, lakini hasukubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliwaomba kuchagua, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni michango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263

Ukituma mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandika: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliwaomba kuchagua, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.



Lipa kwa Simu

Lipa kwa kusan



Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI



‘Msimchoshe Rais Samia kwa usanii’

Na Igo AI

LEO Mzee Tai kaamka vibaya. Siku limeanza kwa “wingu jeusi” kwake! Maana amesikika tangu chumbani akisonya tu.

Na siyo kusonya tu, pia, anagongagonga ukuta, huku akisikika kunena; “yaani hili sikubali, siwezi kuwa mjinga kiasi hiki. Sikubali, lazima nikemee.”

Siyo kawaida ya Mzee Tai kusikika namna hiyo, lazima kutakuwa na jambo lililomkera, tena kero kubwa, maana mengine hupuuzia tu na kuendelea na maisha yake.

Basi, siku ikianza hivyo, wote ndani ya nyumba ya Mzee Tai hunywea na hawapendi hata kukutana naye upenuni wala kwenye viambaza vya nyumba yake, maana hachelewi “kumuwashwa mtu kofi.” Ni hasira za uzee labda!

Siyo mwandishi wala kijana wake anayesaidia kazi za ndani, wote hujitahidi kumkwepa kwa namna wanayoweza, ili jua lizame.

Masalalee! Mzee Tai akaita; “mwandishi...mwandishi... uko wapi? Njoo hapa. Chukua kalamu na karatasi, hili sitaki mambo yenu ya kompyuta mpakato, nataka uandike hapahapa.”

Haya andika haya nayoeleza na unipe nisome kabla ya kupeleka huko Pambazuko. Nataka ujumbe ufike na nisikie mambo yamebadilishwa. Siwezi kukubali jambo hili likapita hivihivi.

“Ni nani anampa Mama mambo ya hovy, kwanini wanamfanyia hivyo, iweje Rais Samia apoteze muda wake kuja kumsikiliza mtu mmoja au wawili, tena kwa mwezi. Tena ndani ya majiji tu, huku kwetu Nanjilini, na kwa babu zangu Ntwale kijijini, atafika lini...”

... Hivi hawa watu milioni 60 atawafikiaje wote kwa kupanga siku moja kwa mwezi, hivi hao wasaidizi wake wamepagawa na nini, au wanamchezea



Rais Samia. Mchoro wa Emma Peer

shere...?

... Nasema sikubali asilan! Hao wasaidizi wake walioko kila kona ya Tanzania na wanalipwa mapesa mengi wanafanya nini, au wanakula mishahara ya bure...!

...Huko kote kuna watendaji wa maeneo yote au wamefukuzwa kazi, hao wakuu wa wilaya wanafanya nini, je, wakuu wa mikoa nao wametimuliwa lini, je, mawaziri nao hawapo, hadi mama aingie fronti?

...Naona kuna mambo ya hovy yanafanyika na lengo ni kumchosha tu Rais Samia. Hili sikubali, nitasema na hakika nitasema sana...

... Lazima tufike mahali tuone heshima ya kiti cha rais inajikita kwenye mambo mazito na makubwa ya kitaifa – tena ya jumla kwa wote, sasa akienda Lumumba, eti pale wanaita ofisi ndogo ya chama cha CCM, akamsikilize shangazi yangu yule wa Ilala, kuhusu kupotelewa kuku wake, tutakuwa tunamtendea haki rais wetu kweli?

... Hata sijui watatumia njia gani kuwapata hao wenye kero zilizoshindwa kutatuliwa huko chini, yaani sijui akili zetu zimechoka?

... Anewei, ngoja nami nijipange kwenda kumuona kumueleza haya, maana naona ni sanaa tu hapa!

Habari/Kenya

Ruto katikati ya kashfa, Bunge kujadili

Na Mwandishi WETU,
Nairobi

WAKATI vuguvugu la kulalamikia maisha magumu kwa wananchi wa Kenya likishika kasi - na bado halijapoa, uongozi wa serikali ya Rais William Ruto umezama katika tope la kashfa ya kutumia fedha bila idhini ya Bunge.

Zaidi ya miezi minne sasa, wananchi wa Kenya kutoka maeneo mbalimbali, hasa kwenye miji mikubwa wamekuwa wakiandamana kupaza sauti zao, wakilaani matumizi makubwa ya serikali ambayo wanaamini yanasababisha maisha yao kuwa makubwa.

Maandamano hayo yamekuwa yakiendelea, huku wananchi wakibeba mabango kuonesha hasira zao kwa serikali kushindwa kudhibiti mfumuko wa bei.

Wengi wamekuwa wakitaja bei ya unga kuendelea kupaa, hivyo kufanya familia zao kulazimika kula milo miwili ama mmoja kwa wengine.

Hata hivyo, serikali kupitia mawaziri wamekuwa wakieleza kwamba bei ya unga imepungua kwa kiasi, na kuahidi kwamba itapungua zaidi na zaidi ili kutoa afueni kwa watumiani. Unga wa mahindi ndiyo chakula kikuu kwa Wakenya.

Wakati wananchi hao wakilalamikia bei ya unga kukomazwa na matumizi makubwa ya serikali; hasa kwa kununua magari ya kifahari, safari za mara kwa mara kwa maofisa wa serikali nje ya nchi, imefahamika kuwa zaidi ya Shilingi za Tanzania Trilioni 1.6, zilitumika bila idhini ya Bunge.

Kiasi hicho ambacho ni Shilingi za Kenya bilioni 70.41 zinaelezwa kutumika katika miradi isiyokuwa ya maendeleo bila idhini ya Bunge katika miezi sita ya kwanza katika mwaka wa kifedha wa 2023/2024.

Mdhibiti wa Bajeti Dkt. Margaret Nyakang'o wiki iliyopita alisema fedha



Rais William Ruto

hizo zilitumika kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFM Act) 2012 inayoeleza kwamba ni lazima Bunge litoe idhini kabla ya serikali kutumia kiasi chochote cha fedha.

Dkt. Nyakang'o alieleza jinsi ambavyo wizara, idara na mashirika ya serikali yalitumia pesa hizo kugharimia shughuli za kila siku badala ya maendeleo. Kwamba fedha hizo hazikugusa manufaa ya moja kwa wananchi, bali viongozi wa serikali.

"Inasikitisha kuwa jumla ya Shilingi bilioni 70.41 zilitumiwa na serikali kuu katika kipindi cha miezi sita bila idhini ya Bunge, hali ambayo inakiuka kipengele cha 223 cha Katiba," Dkt. Nyakang'o amesema na kuongeza kwamba hali hiyo haikubaliki.

Kutokana na matumizi hayo makubwa yasiyoidhinishwa, utulivu wa urais wa Ruto unaelezwa kuendelea "kutetereka" na kuwa ikiwa hali hiyo itaendelea hivyo, kuna wasiwasi kiongozi huyo akalazimika kubadili wasaidizi wake.

"Kinachokwamisha ustawi wa uongozi wa Rais Ruto ni kuongezeka kwa rushwa na matumizi mabaya na makubwa ya wasaidizi wake, tena kwa fedha za walipakodi, sasa hasira ni kubwa kwake, ajipange," amesema Gadi Omondi wa Nairobi.



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Mezani kwa Chahali

Rais Samia siku moja inatosha kweli?

WIKI iliyopita, Rais Samia Suluhu Hassan, alifanya mabadiliko ya viongozi mbalimbali katika ngazi za mikoa na wilaya.

Kwa kiasi kikubwa mabadiliko hayo yalihusu viongozi kubadilishana vituo vya kazi, huku wachache wapya wakiingia katika nafasi.

Kwa kuangalia mabadiliko hayo yalivyopokelewa kwenye mitandao ya kijamii, yayumkinika kuhitimisha kuwa baadhi ya wananchi wana shaka kama mabadiliko hayo yataweza kuchochea ufanisi katika maeneo husika.

Mabadiliko hayo yametokea siku chache tu baada ya Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, kutangaza kwamba mwenyekiti wa taifa wa chama hicho, Rais Samia, atatenga siku moja kwa mwezi kusikiliza kero za wananchi.

Ni jambo zuri kuona kuwa licha ya wingi wa majukumu yake, Rais Samia anaweza kutenga siku moja kusikiliza kero za wananchi. Inamaanisha anawajali wananchi.

Hata hivyo, kuwajali wananchi ni kitu kimoja, na ufanisi katika kuwajali huko ni kitu kingine.

Kwa mfano, japo wazo la rais kusikiliza kero za wananchi ni zuri, lakini ni vigumu kuona likiwa na ufanisi kutokana na ukweli kwamba Tanzania ina jumla ya watu zaidi ya milioni 60. Sasa hata kama watu 1,000 tu wakipata fursa ya kuwasilisha kero zaidi kwa Rais Samia, inaweza kuchukua miaka kadhaa kuwasikiliza wote.

Lakini kimsingi, hakukuwa na haja ya kumwongezea Rais Samia jukumu la kusikiliza kero za wananchi ilhali kuna mlolongo mkubwa wa viongozi ambao, siyo tu wanaweza kusikiliza na kutatua



Rais Samia Suluhu Hassan

kero husika, bali pia wanalipwa mshahara kwa kazi hiyo.

Kwa mfano, endapo changamoto katika ngazi ya mtaa zingeweza kutatuliwa na viongozi wa serikali ya mtaa, ni wazi Rais Samia asingelazimika kutenga siku moja kwa mwezi kusikiliza kero za wananchi.

Hata kama kero za ngazi ya mtaa zisingeweza kupatiwa ufumbuzi katika ngazi hiyo, uongozi wa kata, tarafa, ngazi ya wilaya, mkoa na hatimaye wizarani, zingeweza kutatua tatizo husika badala ya kumlazimu kiongozi wa nchi kushughulikia.

Kuna changamoto kama kwenye maeneo mengine ya serikali, mara kadhaa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amesikika akitoa maagizo kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kufanya uchunguzi au kuchukua hatua dhidi ya watendaji mbalimbali.

Unabaki kujiuliza, hivi Takukuru wanafanya kazi gani hasa mpaka wasubiri maelekezo kutoka kwa waziri mkuu au viongozi wengine wa juu yake?

Kadhalika, viongozi ngazi ya wilaya na mkoa wako wapi hadi kumbidi waziri mkuu kuingilia kati kuwapa maelekezo kutekeleza majukumu yao?

Wasiliana na Chahali kupitia Barua pepe: evarist@chahali.com

Habari**Tanzania yashinda kesi. Kulipwa mabilioni**

Na Mwandishi WETU

KUMEKUWA na vilio na kelele nyingi kutoka kwa Watanzania kila wanaposikia serikali yao “imebwagwa” katika kesi za madai dhidi ya wawekezaji kwenye mahakama za kimataifa.

Katika kesi nyingi, Tanzania imekuwa ikipoteza na kulazimika kulipa fidia nyingi kwa wawekezaji wanaposhinda.

Hata hivyo, wiki iliyopita, Tanzania imeibuka kidedea kwenye kesi iliyokuwa ikiendeshwa katika Baraza la Kimataifa la Biashara (ICC) dhidi ya Kampuni ya Alchemist Energy Trading DMCC kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu.

Uamuzi wa kuipa Tanzania ushindi katika Shauri la Usuluhishi Na. 2682/AZO, baina ya Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (Petroleum Bulk Procurement Agency-PBPA) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya kampuni hiyo, umetolewa na ICC Machi 6, 2024.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, imeliambia Pambazuko kuwa shauri hilo lilifunguliwa baada ya Kampuni ya Alchemist Energy Trading DMCC kushindwa kusambaza mafuta kwa mujibu wa mkataba uliotokana na zabuni Na. PBPA/CPP/PMC/C3-KOJI/02/2021 wa Januari 5, 2021 kwa ajili ya kuleta nchini mafuta, metriki za ujazo 36,192.

Mafuta hayo yalipaswa kupokelewa nchini kuanzia Februari 27, 2021 hadi Machi 1, 2021.

Jopo la utetezi katika shauri hilo liliongozwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akishirikiana na mawakili wengine kutoka ofisini kwake, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na PBPA.

Katika uamuzi wake, Baraza limetamka bayana kuwa Kampuni ya Alchemist Energy Trading DMCC ilivunja mkataba na hivyo likaamuru kurejesha fedha kwa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa



**Wakili Mkuu wa Serikali,
Dkt. Boniphace Luhende,**

Pamoja (PBPA), dola za Marekani milioni 9.7 pamoja na riba kabla ya tuzo (pre-award interest) ya asilimia 7.67 kuanzia Mei 18, 2021 hadi Novemba, 2023; kwa kuvunja mkataba na kushindwa kuleta mafuta nchini.

Baraza hilo mbali na kuamuru Tanzania kurejeshewa fedha hizo, kampuni hiyo imeamriwa pia kulipa PBPA dola za Marekani milioni 1.14 (karibu Shilingi bilioni 2.9) kama adhabu ya kuharibu mfumo wa ununuzi wa mafuta.

Kampuni hiyo pia inatakiwa kulipa PBPA dola za Marekani 882,000 (zaidi ya Shilingi bilioni 2.2) kufidia gharama ilizotumia kuendesha kesi kwenye baraza na pia kulipa gharama za kesi zinazofikia Dola za Marekani 818,285,700.00.

Pambazuko limeelezwa pia kuwa kampuni hiyo pia inatakiwa kulipa riba baada ya tuzo (post award interest) asilimia 7.67 kuanzia uamuzi ulipotelewa Machi 6, 2024 hadi itakapokamilisha malipo yote inayodaiwa.

Akizungumza na Pambazuko jana kuhusu ushindi huo, Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende, amesema “haki imechukua mkondo wake.”

Amesema, katika kesi hiyo, Tanzania ilikuwa na kila ushahidi na kwamba mawakili walikuwa wamejiandaa vyema kutetea maslahi ya Watanzania.



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Tusikubali kuwa taifa la kulalamika

KUNA utamaduni umeanza kuchipuka, kina sasa unastawi kwa kasi, kiasi kwamba, bila kuwoko na jitihada za kuufyekelea mbali, utatia doa nchi yetu mbele ya uso wa jumua ya kimataifa.

Mfano ukimsikiliza na kumtazama kwa makini Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga kwenye kipande cha video cha dakika 3:18, unaweza kupata picha ya watendaji wa serikali wasivyowajibika ipasavyo.

Kinachouma zaidi ni kwamba, kutowajibika ipasavyo huko hakuishii kwenye ofisi za umma walizokabidhiwa, bali kunakwenda mbali hadi kuathiri utumishi wao kwa Watanzania.

Watumishi wabovu waliojaa “roho mbaya” kama alivyosema Sendiga alipokuwa akizungumza na wafanyakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, ndiyo wamejaza ofisi za serikali za kutoa huduma.

Sitaki kurudia neno kwa neno kutoka kwenye hotuba ya mkuu huyo wa mkoa kuhusu masikitiko yake kwa baadhi ya wakuu wa idara wilayani humo ya kujipa ‘Uungu’ na kufikia hata kuzuia stahiki za watumishi bila sababu za msingi.

Lakini hoja yangu ni kuonesha jinsi nchi yetu inavyogeuka taratibu kuwa ya kizazi cha kulalamika kuanzia kwa wananchi wa kawaida hadi kwa viongozi waliotarajiwa kwa mamlaka makubwa waliyonayo, wanguweza kuchukua hatua kutatua changamoto hizo.

Mwanzoni mwa mwaka jana Mkuu wa Mkoa Lindi, Zainab Telak, alilalamikia kitendo cha baadhi ya watendaji kwenye wilaya za mkoa huo kuruhusu kuingizwa kiholela idadi kubwa ya mifugo na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

Telak kupitia mitandao ya jamii, ukiachiliambali uharibifu huo wa mazingira, lakini alionekana amechoka kupokea malalamiko ya migogoro inayotokana na uingizaji holela wa



Waziri wa Utumishi - George Simbachawene

mifugo mkoani mwake kuliko idadi ya maeneo yaliyotengwa kwa matumizi hayo.

Kana kwamba haitoshi, Oktoba 12 mwaka jana, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila akiwa kwenye ziara ya kushitukiza alitushangaza tulipoona naye akilalamika kuona mabasi 70 kati ya 210 ya mradi wa mabasi yaendayo kasi jijini Dar es Salaam (DART) yakiwa mabovu!

Nimejaribu kutoa mifano hiyo michache kuonesha namna wakubwa hawa pamoja na kuchukizwa na utendaji mbovu wa wasaidizi wao, lakini wanakosa nguvu ya kisheria ya kuwajibisha!

Leo inafika mahala mkuu wa wilaya hazungumzi vizuri na mkurugenzi wake, katibu mkuu wa wizara ‘aziwivi’ na waziri wake, naibu katibu mkuu na katibu mkuu utadhani wanaogombea mke, hawapatani. Hapa unatarajia maajabu gani ya kiutendaji?

Ni vyema kuwe na sheria inayowataka viongozi kuwajibishwa itakapobainika, uzembe unaotokana na “kukatika kwa maelewano” miongoni mwao na hapo huenda gonjwa hili likatibika.

Rashid Mtagaluka na Mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari; 0784 438 546 au Email: mtagaluka@gmail.com

Habari

Maisha ya wanafunzi hawa hatarini

Na Mwandishi MAALUM

AFYA za wanafunzi wa Shule ya Msingi Mlevo iliyopo katika Kijiji cha Kilomeni, Wilaya ya Mwanga, Kilimanjaro, zipo hatarini kutokana na uchakavu wa madarasa wanayotumia, kujaa kwa vyoo na kushambuliwa na funza.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wazazi wa wanafunzi wanaosoma katika shule hiyo, wamesema tangu shule hiyo ijengwe mwaka 1975 haijawahi kufanyiwa ukarabati wa aina yoyote.

Mmoja wa wazazi, Stela Mcharo amesema mazingira ya wanafunzi kujisomea shuleni hapo siyo mazuri na baadhi miguu yao 'huliwa' na funza wanaokaa kwenye vumbi la madarasani.

"Mimi ni mzazi ninayesomesha watoto hapa, nasikitika sana kwa hii shule yetu, haina madirisha wala milango, majengo ya shule ni chakavu, watoto wanaliwa funza," amesema mzazi huyo.

Mcharo amemuomba Rais Samia Suluhu Hassan asikie kilio chao.

"Watoto wetu wanapata taabu sana, hawana pa kusomea hata hawa walimu ambao wapo hapa wanafundisha pia funza wanawaingia miguuni." Alipotafutwa kwa simu,

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, Zahara Msangi aliomba apewe muda kwenda kuangalia hali ilivyo katika shule hiyo na kwamba yeye na na timu yake wameelekea kuangalia hali ilivyo katika shule hiyo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kilomeni, Joseph Msangi amekiri kuwepo kwa uchakavu wa miundombinu ya shule hiyo na kwamba mara kadhaa wamekuwa wakitafuta wafadhili kuibuka changamoto za hapa na pale.

"Nimepambana na uongozi wa halmashauri ya kijiji na diwani wa kata



Moja ya madarasa yasiyofaa kutumika shuleni Mlevo

hii angalau tupate fedha au wafadhali wa kutusaidia kujenga hii shule kwa sabau siku zote imekuwa ni chakavu, lakini bado kuna changamoto zinazojitokeza," amesema.

Akizungumzia changamoto ya miundombinu ya shule hiyo, Diwani wa Kata ya Kilomeni, Mohammed Mgala, amesema Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule hiyo lakini hakuna kinachotekelezeka.

"Shule hii ilianza mwaka 1975 wakati wa UPE (elimu ya msingi kwa wote) ili kuwezesha wanafunzi kwenda shule, kwa hiyo ilijengwa kwa taratibu ambazo si za viwango na ndio imetufikisha hapa tulipo.

"Tunashukuru Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya kujenga shule hii lakini haijengwi, mwaka jana shule hii ilipewa Sh50 milioni, mwaka huu imepewa Sh67 milioni kwa ajili maboresho mbalimbali lakini haijengeki," amesema Mgala ambaye pia ni makamu mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya hiyo.

"Shule imepewa fedha za vyoo zaidi ya Shilingi milioni 10, lakini mpaka sasa hakuna kilichofanyika," ameongeza Mgala, bila kufafanua fedha hizo zimekwenda wapi.

Habari hii imechapishwa kwa sababu maalum. Imeandika kwa mara ya kwanza na gazeti la Mwananchi - Mhariri

Saa 67 zamtoa jasho Silaa kero za ardhi

Na Mwandishi WETU

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa kwa siku sita mfululizo, amesikiliza, kuelekeza na kutatua baadhi ya changamoto na kero za “minyukano” ya ardhi katika maeneo ya Bunju, Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam.

Katika siku hizo, akiwa amehamishia ofisi yake Uwanja wa Shule ya Msingi Bunju A, Silaa alitumia wastani wa saa 11.20 kila siku, hivyo kufanya jumla ya muda aliotumia kusikiliza wananchi kuhusu migogoro ya ardhi kufikia saa 67.

Silaa, kuanzia mwishoni mwa Februari hadi wiki iliyopita, akiwa ameambatana na baadhi ya wakurugenzi na maofisa waandamizi wa wizara anayoongoza, amefanya vikao mfululizo na wananchi wa Bunju ambao wamekuwa na changamoto za ardhi.

Pambazuko ambalo lilikuwepo kufuatilia utendaji wa wizara hiyo na namna inavyotatua kero, changamoto na shida za wananchi, lilishuhudia kero kubwa ikiwa ni kucheleweshwa kwa upatikanaji wa hati.

Wananchi wengi waliomfikia Silaa walieleza kukerwa na hata baadhi kukata tamaa ya kuzungushwa ndani ya wizara anayoongoza, kwa zaidi ya miaka saba wakihangaikia hati zao, hata baada ya kuwa wamekamilisha taratibu zote, ikiwamo kulipia gharama zote za serikali ili kutwaa ardhi.

Katika muda wa ofisi ya Silaa kuhamia Bunju, wapo baadhi ya wananchi walifanikiwa kutatuliwa kero zao za migogoro ya ardhi, na wengine wakipatiwa hati za umiliki wa ardhi pale pale uwanjani.

Kero nyingine kubwa ambayo Silaa alilazimika kuagiza na kuonesha ukali, ni kampuni binafsi zilizopewa kandarasi ya kupima na kukusanya taarifa, kusuasua



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa

kukamilisha kazi hiyo kwa zaidi ya miaka sita sasa.

Silaa alilazimika kutoa wiki tatu kwa kampuni hizo kuhakikisha zinakamilisha nyaraka zote na kuzifikisha kwa watendaji wa wizara yake ili kupata muafaka na kwa wenye sifa na kukamilisha taratibu kuata hati zao haraka.

“Inasikitisha kuona usugu wa jambo hili, kila mwaka na kila waziri anayekuja anakuta migogoro mingi ajabu, mingine ingeweza kumalizwa kwa siku moja na watendaji wetu, lakini inadumu kwa muda mrefu na kufanya watu kuchukia serikali yao, hili jambo halikubaliki na sasa ni muda wa kutatua,” alifoka Silaa.

Silaa ambaye aliipishwa na Rais Samia Suluhu Hassan Septemba 01, 2023 kuongoza wizara hiyo, amepa “kukomaa zaidi” ili kuhakikisha kuwa changamoto za ardhi, pamoja na wingi na ugumu wake, anazifanya kazi usiku na mchana ili kuzipunguza.

Silaa amewaagiza makamishna wa ardhi wasaidizi wa mikoa yote kujitathmini katika kutekeleza maagizo ya Rais Samia kuhusu matumizi bora ya ardhi na kuhakikisha wanakuwa msaada kwa wananchi badala ya kuwa sehemu ya kero na shida kwa wananchi.

Habari**ACT wajipanga kususia serikali**

Na Waandishi WETU

SASA ni wazi kwamba Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar (SUK) inayoongozwa na vyama viwili; Chama Cha Mapinduzi (CCM) pamoja na ACT-Wazalendo, ipo shakani.

Tayari ACT-Wazalendo kimeweka hadharani msimamo wake kwamba kinakwenda kujitoa kwenye serikali hiyo.

Akitangaza uamuzi huo kwa waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu Ado alisema tathmini ya kina iliyofanywa na halmashauri kuu ya chama chake inaonesha kuwa mbali na suala la kuachiwa huru kwa wanachama waliokuwa wanashikiliwa kutokana na Uchaguzi Mkuu 2020, hakuna hoja hata moja kati ya tatu za mageuzi ya kimfumo zilizotekelezwa hadi sasa na serikali inayoongozwa na Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

Ado anasema hoja zilizokuwa zimekubaliwa awali na pande zote mbili kwa usimamizi wa viongozi wawili ambao ni Rais Dkt. Hussein Mwinyi na Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo wakati huo, Seif Sharif Hamad ni pamoja na kulipwa fidia wahanga wa Uchaguzi Mkuu 2020, Kuundwa kwa Tume ya Kijaji kuchunguza uvunjifu wa haki za binadamu kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 pamoja na kuwapo mageuzi katika mfumo wa uchaguzi.

“Halmashauri Kuu ya Chama Taifa – ACT Wazalendo kwenye kikao chake cha Machi 4, 2024 ilitoa agizo kwa Kamati ya Uongozi Taifa kuonana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar kuwaeleza juu ya uamuzi wa ACT Wazalendo kujitoa kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) kutokana na kutotekelezwa kwa makubaliano yaliyolingiwa na Maalim Seif kwa niaba ya ACT-Wazalendo na

*Rais Dkt. Hussein Mwinyi*

Rais Mwinyi kabla ya ACT Wazalendo kujiunga na Serikali ya Umoja wa Kitaifa mwaka 2020.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo aliyemaliza muda wake, Zitto Kabwe katika hotuba yake ya mwisho kwenye mkutano mkuu wa chama hicho uliofanyika Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam wiki iliyopita, alimuomba Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana kuwa amwambie Rais Dkt. Mwinyi afungue mikono yake ili Zanzibar iweze kutawalika.

“Juhudi za maridhiano Zanzibar hazijazaa matunda, nilishiriki vikao vya maridhiano, tulifanya moyo mgumu kuingia kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa baada ya kupoteza watu 24 waliofariki dunia kwenye uchaguzi huo na wengine wamebaki vilema hadi leo”

“Mheshimiwa Kinana naomba utupelekee salaam zetu kwa Rais, Zanzibar haiko sawa, tondoe hii violence (mateso) wakati wa uchaguzi, Wazanzibar wapige kura yao bila kupoteza maisha.

Akizungumza na Pambazuko kuhusiana na suala hilo, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dkt. George Kahangwa alisema suala la Serikali ya Umoja wa Kitaifa liko kwa wananchi wa Zanzibar, kamwe siyo la vyama vya siasa.

Inaendelea Uk. 13

ACT wajipanga kususia serikali

Inatoka Uk. 12

Amesema SUK ni sehemu ya lazima ndani ya Katiba ya Zanzibar, hivyo ameshauri vyama hivyo virudi kwa wananchi na kuwauliza wanataka nini juu ya suala hilo.

Dkt. Kahangwa alisema hatua ya chama cha ACT -Wazalendo kutaka kukutana na marais wa pande zote mbili kutafuta muafaka wa SUK ni jema na msingi sana kuliko uamuzi wa kujitoka kwenye serikali hiyo.

Amesema kujitoka katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa siyo dawa ya kukomesha kile alichaita dhuluma za watawala, huku akitolea mfano mwaka 2015 ambapo aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jecha Salim Jecha (sasa marehemu) alipofuta matokeo ya Uchaguzi Mkuu ambapo mgombea Urais wa Chama Cha Wananchi (CUF) wakati huo, Maalim Seif Sharif Hamad alidhaniwa ameshinda uchaguzi huo.

“Baada ya uamuzi huo wa Jecha, Maalim na chama chake walijitoka kwenye kinyang’anyiro hicho, lakini haikusaidia kwani CCM iliendelea kuongoza serikali bila kujali kilichotokea.

“Uchaguzi mkuu wa 2015 ni funzo tosha baada ya Jecha kufuta matokeo, Maalim Seif na chama chake cha CUF walijitoka, lakini haikusaidia kuwazuia CCM kutawala. Njia iliyo sahihi ni hii ya kuonana na marais hao na kufanya majadiliano na kupata muafaka” amesisitiza Dkt. Kahangwa.

Hata hivyo, msomi huyo aliongeza kusema kuwa kwakuwa nchi ipo kwenye majira ya uchaguzi, hoja hiyo ya kujitoka au kutokujitoka katika SUK ni kete ya kuingilia kwenye kampeni za uchaguzi huo kwa kuipeleka kampeni mahakama ya kisiasa ambayo ni wananchi.

Fatma Karume alonga

Akizungumzia kuhusu tishio la ACT-

Wazalendo kujitoka kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa, wakili maarufu nchini ambaye pia aliwahi kuwa Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Fatma Karume amesema jambo hilo halikumshangaza kwa sababu historia inaonesha serikali hiyo haijawahi kufanya kazi pamoja.

Fatma ambaye pia ni mtoto wa Rais (mstaafu) wa Zanzibar, Amani Abeid Karume alisema rais aliyeshika mpini ameshindwa kufanya kazi na wenzake.

“Mambo mengi yanahitaji hekima na busara ya rais, kwamba lazima sera za upande wa pili ziwekwe kwenye uwajibikaji ili kuwe na usawa, siyo kunakuwa na SUK halafu sera inayofuatwa ni ile ya rais aliyeko madarakani, haiko hivyo kabisa...

“Tena rais aliyeshika mpini ndio anatakiwa kuwa mnyenyekevu kwelikweli, siyo wa upande wa pili ndio wawe wanyenyekevu, sasa kwa kuwa ameshindwa hayo na kashindwa kuchukua maoni ya wenzake, ndio maana imetokea matatizo haya,” amesema Fatma.

Kuhusu Zanzibar itakuwaje bila SUK, wakili huyo amesema ingawa serikali iliyopo madarakani itaendelea kuongoza, lakini dunia itakuwa imefahamu kwamba rais aliyeko madarakani kashindwa kufanya kazi na wenzake.

Mbobezi wa sheria na mwanaharakati wa haki za binadamu, Dkt. Hellen Kijo Bisimba, naye amesema SUK isingedumu kwa sababu upande mmoja una nguvu na ndio ulioko madarakani, huku mwingine ukionekana dhalili.

Amesema ni dhahiri hadi ACT-Wazalendo kufikia hatua ya kutishia kujitoka, inaonesha wameshakanyagwa sana ndani ya huo umoja kwa sababu sera zinapingana, hivyo lazima wangejitoka tu.

“Hakuna umoja wa aina hiyo kwamba

Inaendelea Uk. 18

Tangazo



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au

Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

‘Bandari ziko vizuri, hakuna hujuma’

Na Mwandishi WETU

UFANISI wa kazi na huduma katika bandari zote za Tanzania uko katika kiwango cha juu, baada ya kuwepo kwa maboresho yanayoendelea ili kukidhi mahitaji ya wateja wote; wakubwa kwa wadogo.

Hakikisho hilo limetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa wakati akizungumza na Pambazuko, huku akiomba wananchi kupuuzwa habari hasi zinazosambazwa mitandao kuhusu Bandari ya Dar es Salaam.

Mbossa amesema tangu kuanza kwa huduma za bandari nchini, hivi sasa huduma zinazotolewa zinaendana na wakati na mabadiliko ya teknolojia na kwamba katika maboresho hayo, maslahi ya wafanyakazi nayo yanaendelea kuboreshwa.

Anasema taarifa zilizosambazwa katika mitandao ya kijamii na makundi sogozi kuhusu madai ya kuwepo mgomo wa wafanyakazi na baadhi kupunguzwa kazi katika Bandari ya Dar es Salaam, zinapaswa kupuuzwa kwani hazina chembe ya ukweli na zinasambazwa kwa nia ovyu.

Mbossa anasema maboresho yote yanayofanyika hadi sasa katika Bandari ya Dar es Salaam, ni kuhakikisha huduma za uendeshaji zinaendelea kuwa bora zaidi chini ya TPA kabla ya kuanza kazi kwa Kampuni ya DP World kutoka Emirate, yenye makao makuu Dubai.

Pambazuko linatambua kwa kuthibitisha kuwa maboresho makubwa ya miundombinu yaliyofanyika katika Bandari ya Dar es Salaam, yameiwezesha bandari hiyo kuwa na uwezo wa kuhudumia meli kubwa na za kisasa zenye urefu hadi kufikia mita 305.

Kwamba kabla ya ukarabati huo,



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania, Plasduce Mbossa

bandari hiyo ilikuwa na uwezo wa kuhudumia meli zenye urefu wa mita zisizozidi 250 na ikitokea ikiingiza meli kubwa zaidi hazizidi mita 300.

Aidha, kina cha maji katika Bandari ya Dar es Salaam kimeongezwa, hivyo kuimarisha zaidi magati ambayo kwa sasa yana uwezo wa kuhudumia meli kubwa zaidi na zenye urefu mkubwa bila mkwamo wala kuhitaji usaidizi wa mashine zingine.

Sambamba na maboresho hayo, Bandari ya Dar es Salaam imeongeza kina kwenye magati yake hadi kufikia urefu wa mita 14.5 kwenye gati namba 1 hadi 7.

Mbali ya kuboreshwa kwa magati hayo, eneo la kugeuzia meli limeongezwa upana hadi kufikia mita 520 ili kuwezesha meli za kubwa zaidi kuingia bandarini kwa urahisi.

Zaidi sana, Pambazuko limeshuhudia maboreho katika lango kuu la meli kuingia bandarini pia limechimbwa na kuwa na urefu wa kina cha mita 15.5 pamoja na upana wa mita 200.

Bandari ya Dar es Salaam ni moja kati ya bandari mama zinazoendeshwa na kumilikiwa na serikali kupitia TPA. Bandari nyingine ni pamoja na Bandari za Tanga na Mtwara, ambazo nazo zinaendelea kuboreshwa ili kuhudumia wateja wengi zaidi kwa ufanisi.

Uchambuzi

Dira ya Taifa 2050; tunapanga kushindwa?

Na Mwandishi WETU

MIPANGO ya kiuchumi ya nchi inaongozwa na Dira ya Taifa ili kufikia malengo yanayokusudiwa kwa kipindi fulani.

Hivi sasa Tanzania inakamilisha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya mwaka 2025.

Utaratibu huu wa kuwa na Dira ya Taifa ulibuniwa mwishoni mwa uongozi wa awamu ya pili chini ya Rais Ali Hassan Mwinyi na kuanza utekelezaji katika awamu ya tatu, wakati huo rais akiwa Benjamin Mkapa.

Dira ni chombo cha kuongoza mwelekeo wa maendeleo kwenye nyanja zote katika taifa katika kipindi cha muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Ndio maana utekelezaji wa Dira ya Taifa hugawanywa katika vipindi vya miaka 25, miaka mitano na hata mwaka mmoja mmoja.

Katika miaka 25, kunakuwa na lengo kuu la jumla linaloonesha maendeleo ya nchi yanapaswa kufikia wapi katika kipindi hicho.

Ili kulifikia lengo hilo utekelezaji wa mipango hiyo ya maendeleo hugawanywa katika kipindi cha miaka mitano mitano.

Ndani ya kila miaka mitano, kunakuwa na mpango wa mwaka mmoja mmoja ambao hutekelezwa kupitia bajeti katika mwaka wa fedha husika.

Hivyo, kimsingi, yale tunayoeleza katika bajeti ya kila mwaka, ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya miaka mitano na miaka 25.

Mchakato wa kuandaa dira ya maendeleo nchini ulianza mwaka 1994, mwaka mmoja kabla Rais Mkapa hajaingia madarakani.

Mchakato huo ulikamilika na dira kupitishwa mwaka 1999 na utekelezaji wake ukaanza kupitia bajeti ya waka wa fedha uliofuata, 2000.

Kwa kawaida, uandaaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa unapaswa kuhusisha



Rais Samia Suluhu Hassan

makundi yote katika jamii, kwani hakuna kundi ambalo halihusiki na maendeleo.

Pamoja na hayo, ushirikishwaji huu mpana unalenga kuipatia dira hiyo uhalali wa kuwa chombo kinachotumika kwa ajili ya maendeleo ya wote.

Kwa maana hiyo, utekelezaji wa dira hiyo uhusisha kila Mtanzania. Dira inapoweka malengo kuwa ifikapo mwaka fulani kila mwananchi awe na maisha bora.

Hakuna mtu mwingine kutoka mahali pengine ambaye atakuja kutekeleza mipango ya kumfanya kila Mtanzania awe na maisha bora, isipokuwa mwananchi mwenyewe.

Ukiacha ushirikishwaji wa wananchi wote, jambo jingine kubwa inapoandaliwa Dira ya Taifa, ni tathmini ya dira inayomaliza muda wake.

Ni lazima kufanya tathmini ya dira inayomalizika ili kupima mafanikio yake kwa lengo la kuhakikisha kuwa yanaendelezwa.

Pia, tathmini ya dira inayomaliza muda wake, ni muhimu ili kubaini mambo yaliyokwaza utekelezaji wa dira hiyo.

Mambo haya yanawezesha kuandaa dira mpya ambayo inatoa suluhisho kwa vikwazo na changamoto zozote zilizoibuka wakati wa utekelezaji wa dira inayomaliza muda wake.

Kwa kuwa mwaka 1994 ilipoandaliwa dira ya kwanza ya maendeleo hakukuwa na dira nyingine kabla yake, naamini

Inaendelea Uk 17

Dira ya Taifa 2050; tunapanga kushindwa?

Inatoka Uk. 16

tathmini ilifanyika kwa kuzingatia hali ya uchumi wakati huo na kuona ni wapi Tanzania inapaswa kuelekea.

Ni lazima tathmini ilifanyika kwa sababu bila hiyo ingekuwa vigumu kuweka vigezo vya nini kinatakiwa kufanyika na kifanyike vipi ili kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa.

Lakini, kitu cha ajabu ni kuwa mchakato wa kuandika Dira ya Taifa ya mwaka 2050 umeshaanza huku tathmini ya Dira ya Mwaka 2025 ikiwa haijakamilika.

Kazi ya kufanya tathmini hiyo ilitolewa kwa taasisi moja ya utafiti wa masuala ya umasikini Tanzania, inayoitwa REPOA, lakini hadi wiki iliyopita ripoti mahsusi ya tathmini ya utekelesaji wa Dira ya Taifa 2025 ilikuwa bado haijakamilika.

Kuanza kuandaa mipango mipya bila kujua vigezo hivyo ni sawa na kufanya mapishi bila kuwa na viungo muhimu. Kuna hatari ukapika mchuzi ambao ladha yake haitajulikana vizuri.

Hii ina maana kuwa nchi inapoanza kupanga Dira ya 2050 bila ya kuwa na tathmini ya dira inayomalizika, ni sawasawa kabisa na kupanga kushindwa.

Dira inayomalizika ilikuwa na malengo matano makubwa.

Lengo la kwanza lilikuwa ni kuleta maisha bora kwa Watanzania wote. Chini ya dira ihiiyo ilipangwa kuwa hadi kufikia mwaka 2025, kila mtanzania awe na maisha bora na pasiwepe ma Mtanzania masikini.

Dira ililenga uwepo wa huduma bora za afya, elimu, maji, miundombinu, umeme, skimu za umwagiliaji na huduma nyinginezo za kiuchumi na kijamii.

Lakini, ni dhahiri kuwa hayo hayajaitimia kwa sababu huduma za jamii bado ni duni katika maeneo mengi na idadi ya masikini nchini, bado ni kubwa na kiwango cha umasikini ni kikubwa katika maeneo mengi.

Lengo la pili lilikuwa ni kuhakikisha



Waziri wa Mipango - Prof. Kitila Mkumbo

kuwepo wa amani, utulivu na umoja. Utulivu wa kisiasa ni moja ya mambo ambayo yalilengwa kufikiwa ili kuwa na nchi yenye amani ya kweli.

Hivi sasa tunashuhudia mivurugano ya kisiasa inayoendelea nchini. Chadema na vuguvugu lao na madai ya katiba mpya na mabadiliko ya sheria za uchaguzi, huku ACT-Wazalendo ikieleza dhamira yake ya kujitoa katika serikali ya umoja wa kitaifa huko Zanzibar.

Tatu Dira ililenga kujenga utawala bora nchini. Sote ni mashahidi jinsi hata viongozi waliopo madarakani wanavyoibua mambo ambayo yanaonesha kutokuwepo kwa utawala bora.

Lengo la nne lilikuwa ni kuhakikisha uwepo wa jamii iliyoelimika na yenye kujifunza. Sote tu mashahidi jinsi elimu yetu ilivyoendelea kuwa kitu cha majaribio miaka nenda miaka rudi.

Tano tulipanga kupitia Dira ya 2025 kuhakikisha Tanzania inakuwa na uchumi imara na shindani kwa mataifa mengine. Hili ni kama limeshindikana.

Nchi inajinasibu kuwa inajenga uchumi wa viwanda, lakini hadi leo bado tunatumia sehemu ndogo ya soko la Marekani kupitia AGOA kwa sababu hatuna viwanda vya kutosha kuzalisha bidhaa kwa ajili ya soko hilo.

Tukutane wiki ijayo ambapo baada ya kufanya tathmini binafsi na kuleta mapendekezo ya nini kinapaswa kupewa msisitizo kwenye Dira ya Taifa ya 2050.

Habari

Mradi wa SWIL ulivyoibua ‘makubwa’

Na Jabir Idrissa

UTEKELEZAJI wa mradi wa SWIL - “Imarisha Wanawake kwa ajili ya Uongozi” unaofadhiliwa na Norway, umeibua hamasa kubwa ya wanawake kutambua haki zao za kiraia na kikatiba pamoja na kufichua vipawa kwa waandishi chipukizi.

Kwenye mahojiano maalum na Pambazuko jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (Tamwa) Zanzibar, Dkt. Mzuri Issa amesema kupitia mradi huo uliotimiza miaka minne tangu kuanza kwake, wanawake wameongezeka kupata muamko wa kuzitambua haki zao ikiwemo kugombea nafasi za uongozi katika vyombo vya uamuzi nchini.

Dkt. Mzuri ambaye kitaaluma ni mwandishi wa habari na mwanamawasiliano, amesema mradi wa SWIL umelenga kuongeza ushiriki wa wanawake katika hatua za kuimarisha demokrasia na uongozi kwa ngazi zote za jamii ili kufikia kutambuliwa kuwa nao ni sehemu muhimu ya kukuza demokrasia

badala ya kuonekana ni wasindikizaji tu au watu wa kupendelewa.

Mradi huo ambao unatekelezwa kwenye wilaya zote 11 Unguja na Pemba, unajumuisha jukumu la kujenga uwezo wanawake kielimu na maarifa yatakayosaidia wajiamini na kujitokeza kushiriki harakati za kugombea nafasi za uongozi kupitia vyama vya siasa ambako ndiko utungaji sera na sheria hufanyika kupitia mabaraza ya miji, halmashauri, bunge na baraza la wawakilishi.

Dkt. Mzuri anasema wakati mradi ukitimiza mwaka wa nne, wanajivunia mafanikio ya kupigiwa mfano ikiwemo kuwezesha wanawake wapatao 500 wa Zabzibar kupata mafunzo ya kujitambua na kupata uwelewa ili kushiriki hatua mbalimbali za kupigania uwakilishi katika vyombo vya maamuzi.

“Tumejionea namna wanawake tena kutoka ngazi ya chini kwenye jamii walivyohamasika na kutambua haki zao ikiwemo ya kugombea uongozi kwenye vyama vya siasa. Isitoshe, mafunzo tunayowapa yamesaidia kuibuliwa matatizo yanayowakabili katika maisha

Mpasuko Zanzibar

Inatoka Uk. 13

upande mmoja una nguvu na sera hazifanani, ni umoja ambao hauna usawa, hata kipindi fulani ulivyodumu, niliona ni ajabu sana ni vile tu Watanзания ni watu wa kumezea vitu, lakini umoja wa aina hiyo hivyo siyo rahisi kabisa.

“Nadhani wameamua kujitoka kwa sababu sera zao zinapingana, kuna wakati hata wakitoa maoni yao wanaonekana wanapinga, “ameongeza Dkt. Bisimba.

Katiba ya mwaka 1984 ambayo ilifanyiwa marekebisho makubwa mwaka 2010 ndiyo iliyoweka kipengele cha Zanzibar kuongozwa kwa Ushirika wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambapo

chama kilichopata kura nyingi za urais, kitashirikiana na chama kilichoweza kufikisha asilimia 10 ya kura hizo za urais.

Ikulu Zanzibar yanena

Ikulu ya Zanzibar ilipoulizwa kuhusu mtazamo wake na namna serikali ilivyojipanga kupokea msimamo wa ACT, kupitia kwa mkurugenzi wake wa mawasiliano, Charles Hillary, iliomba mwandishi kusubiri kauli rasmi ya serikali.

“Serikali mpaka sasa haijatoa kauli yoyote mpaka sasa, subiri kauli ikitolewa majibu yako yatajiibiwa,” amesema Hillary wakati akijibu maswali ya Pambazuko jana.

Arusha yampa ushindi Miss World



Na Mwandishi WETU

MIONGONI mwa chachu za ushindi mwa mrembo wa dunia (Miss World) mwaka 2024, ni makala fupi ya video ikionesha ushiriki wake kupinga ujinga kwa watoto wa Tanzania.

Mshindi huyo, ni Krystyna Pyszková, miaka 24 kutoka Jamhuri ya Czech.

Krystyna ameshinda taji hilo juzi – Machi 9, baada ya kuwabwaga washiriki wengine 111 kutoka mataifa mbalimbali duniani. Mashindano hayo yalifanyika kwenye Ukumbi wa Jio World Convention Centre, jijini Mumbai, India.

Makala iliyosukuma ushindi wake na namna alivyokuwa akielezea alivyopambana kutokomeza ujinga, Krystyna alisema harakati zake ni kuhakikisha kila mtoto anapata elimu, hivyo aliamua kwenda Arusha, Tanzania na kuanzisha shule akishirikiana na Taasisi ya Sonta mwaka 2022. Picha mbalimbali zaonesha akiwa na wanafunzi.

Alisema shule hiyo ilianzishwa kwa lengo la kutoa elimu kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu na

wasiokuwa na wazazi ama walezi wa kulipia gharama.

Krystyna ambaye alikuwa miongoni mwa walimu wa lugha ya Kiingereza shuleni hapo, anazungumza lugha tano kwa ufasaha; Kiingereza, Kipolish, Kijerumani, Kislovakia na Kiarabu kidogo.

Krystyna amepokea taji hilo kutoka kwa aliyekuwa akilishikilia, Karolina Bielawska, raia wa Poland.

Mshindi wa pili wa Miss World ni Yasmina Zaytoun kutoka Lebanon.

Mrembo wa Tanzania, Halima Kopwe, alifanikiwa kuingia 40 bora, nafasi ambayo katika mashindano hayo ilikuwa sawa na robo fainali.

Warembo walioingia 12 bora na nchi zao kwenye mabano ni Kristen Wright (Australia), Maria Victoria Bayo (Jamhuri ya Dominican), Liza Gundowry (Mauritius), Paula Pérez (Hispania) na Lesego Chombo (Botswana).

Wengine ni Leticia Frota (Brazil), Krystyna Pyszková (Jamhuri ya Czech), Jessica Gagen (Uingereza), Sini Shetty (India), Yasmina Zaytoun (Lebanon), Aché Abrahams (Trinidad and Tobago) na Hannah Tumukunde wa Uganda.



Ubabe wa Bil. 126/-...



Bondia Anthony Joshua wa Marekani, amedhihirisha ubabe wake kwa ndondi za uzito wa juu baada ya kumondosha - mara tatu ndani ya raundi mbili, Francis Ngannou katika mchezo wa masumbwi uliochezwa juzi huko Saudia. Ngannou ni mzaliwa wa Cameroon, anayeishi Uingereza. Anthony aliweka kibindoni Shilingi bilioni 76, huku Francis akiondoka na kitita cha Shilingi bilioni 50 baada ya kuzichapa kwa dakika tano. Picha na Getty Images/Richard Pelham.

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

